Hivi sasa sote tumeshuhudia kuwa dunia imekumbwa na mabadiliko makubwa ya tabia nchi yanayosababishwa na shughuli mbalimbali za binadamu na majanga ya aina mbalimbali. Kutokana na hali hii watu wengi hususani wa hali ya chini ndio wamekuwa wahanga wa mabadiliko hayo. Kwa mfano, upatikanaji wa maji salama kwa matumizi ya binadamu, makazi safi na salama umekuwa ni shida kubwa hivyo matumizi ya maziwa mengine badala ya maziwa ya mama haufai kwani ni vigumu kuyaandaa katika hali ya usafi na ukosefu wa maji safi na salama na miundombinu muhimu katika makazi yetu. Katika hali hiyo, unyonyeshaji wa maziwa ya mama ndiyo njia ya pekee ya kulinda afya na uhai wa watoto wachanga.

Ndugu wanahabari,

Sababu kubwa ya utapiamlo kwa watoto ni ulishaji usio sahihi ambao huchangiwa na majukumu mengi yanayomkabili mama na hivyo kukosa muda wa kutosha wa kumtunza mtoto. Ni dhahiri kuwa mchango wa mwanamke katika familia, ajira na uzalishaji kwa ujumla ni mkubwa hivyo ni muhimu kuwatia moyo na kuwasaidia wanawake ili waweze kufanya majukumu ya uzalishaji na utunzaji familia kwa ukamilifu.

Kwa kuzingatia jambo hili nchi yetu imechukuwa hatua mbalimbali kuendeleza unyonyeshaji ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini ya mwaka 2004 inayotambua kuwa unyonyeshaji ni haki ya mtoto na hivyo hutoa mafao mbalimbali ya uzazi ili kuwawezesha

wazazi kumlea mtoto hususani kumnyonyesha ipasavyo. Mama mwajiriwa anayenyonyesha hupewa ruhusa ya masaa mawili kila siku ili akamnyonyeshe mtoto wake. Pia, sheria hiyo hutoa fao la likizo ya uzazi kwa mama na baba wa mtoto. Mama anapata likizo ya siku 84 kama amejifungua mtoto mmoja na siku 100 kwa watoto zaidi ya mmoja. Sheria hii pia humpa baba likizo ya siku 5 ndani ya wiki moja aliyojifungua mama.

Vile vile sheria hiyo inakataza mama aliye ajiriwa na ambaye ananyonyesha au mjamzito kufanya kazi ngumu au za hatari kwa afya yake au ya mtoto wake, kumpangia kazi za usiku na ubaguzi wa aina yoyote. Kwasababu hii, tunatoa wito kwa Taasisi zisizo za kiserikali, Taasisi za kijamii na za kidini, jamii na familia kwa ujumla kuhamasisha na kuwasaidia wanawake ambao wapo kwenye ajira rasmi na zisizo rasmi ili waweze kuwanyonyesha watoto wao ipasavyo. Aidha tunaomba jitihada za dhati zifanyike ili kuwapatia nafasi/eneo wanawake wanaonyonyesha waweze kunyonyesha watoto wao wakiwa katika maeneo yao ya kazi. Tuige mfano wa ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Dodoma kwani wameonesha kuwajali wamama wanaonyonyesha watoto wao kwa kutenga eneo maalum kwa ajili ya mama wanaonyonyesha.

Ndugu wanahabari,

Ili kufanikisha unyonyeshaji, sambamba na uzalishaji mali, ajira kwa wanawake yafuatayo yanaweza kufanyika:

- Kusimamia ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria za kazi hususani Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini katika sekta binafsi na serikali
- Kuhamasisha watoa maamuzi ikiwa ni pamoja na wabunge ili kuboresha Sheria ya kazi ili kutoa likizo ya uzazi kwa wiki 14 au zaidi kama inavyopendekezwa na shirika lakazi Duniani.
- Kujenga uelewa kwa wanawake walioajiriwa kuhusu haki ya uzazi katika sehemu zao za kazi
- Kufanya tathmini ya mara kwa mara ya jinsi gani Sheria ya haki ya uzazi inavyotekelezwa katika sehemu mbalimbali za kazi
- Kutenga sehemu maalumu katika sehemu za kazi kwa ajili ya wanawake wanaonyonyesha waweze kuja na watoto wao kazini na kuwanyonyesha kila wanapohitaji au kukamua maziwa yao ili kuepukana na athari za kujaa kwa matiti ikiwa ni pamoja na kupungua utokaji wa maziwa au kukauka maziwa kabla ya mtoto kutimiza miaka 2.

Ndugu wanahabari,

Sote tunatambua dhima ya vyombo vya habari ni kutoa taarifa, kuelimisha na hata kuburudisha. Lakini katika miaka ya hivi karibuni dhima hiyo imepanuka na kujumuisha masuala ya ufuatiliaji, kupaza sauti za watu wasio na sauti katika jamii, kusaidia kulinda maslahi ya jamii na mambo mengine mengi. Vyombo vya habari vina wajibu wa kuendelea kuhabarisha, kuelimisha kuhusu umuhimu na taratibu sahihi za

unyonyeshaji kama vile kuanzisha kunyonyesha mtoto ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, Kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama pekee katika miezi sita bila kumpa kitu kingine chochote, Kumnyonyesha mtoto kila anapohitaji na kuendelea kumnyonyesha hadi anapofikisha miaka miwili.

Halikadhalika, vyombo vya habari vinaweza kufuatilia utekelezaji wa sheria mbalimbali zinazolinda haki za uzazi na ulishaji wa watoto kwa kufanya utafiti, kuandika au kuripoti matukio mbalimbali kama vile ukiukwaji wa haki za uzazi na sheria ambao hufanywa na waajiri, makampuni yanayofanya biashara ya maziwa na vyakula vya watoto hivyo kudidimiza unyonyeshaji wa mtoto. Vile vile vyombo vya habari vinaweza kuwasemea makundi mbalimbali yasiyo na sauti katika jamii hususani watu maskini ili wapate msaada waweze kuongeza kipato chao na kusaidia kuboresha lishe kwa ajili ya familia zao hasa watoto wadogo.

Ndugu wanahabari,

Katika kutekeleza malengo ya wiki ya unyonyeshaji ya mwaka 2018 shughuli mbalimbali zitafanyika ikiwa ni pamoja na uhamasishaji katika ngazi ya Taifa na Mkoa /wilaya kwa kutoa unasihi wa ulishaji wa watoto katika vituo vya afya na maeneo maalum yatakayotengwa katika kila mkoa au wilaya, semina kwa waandishi wa habari, uelimishaji na uhamasishaji wa jamii kupitia vyombo vya habari.

Ndugu wanahabari,

Maadhimisho haya yanaanza rasmi tarehe 01/08/2018 hadi tarehe 07/08/2018. Elimu na taarifa mbalimbali zinazohusu unyonyeshaji na lishe ya watoto kwa ajili ya kujenga msingi imara wa afya na maisha ya watoto zitatolewa wakati wote wa maadhimisho. Mabango na vijarida mbalimbali vyenye taarifa za Unyonyeshaji pia vinapatikana.

Ndugu wanahabari,

Ninaamini kuwa katika kipindi hiki cha maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji duniani mtatumia taaluma yenu kwa kuzingatia nafasi muhimu mliyonayo katika jamii ili kuhamasisha na kuelimisha umma kuhusu utunzaji wa watoto hasa wale wachanga na wadogo ili tupate taifa lenye watu bora wanaoweza kuleta maendeleo hasa tukizingatia lengo la Serikali la kuwa na uchumi wa viwanda. Haya yote yatawezekana endapo kila mmoja ataamua kwa dhati kutimiza wajibu wake ili kulinda na kuendeleza afya na lishe ya watoto wetu kwani ndio msingi wa maisha.

Asanteni Sana kwa kunisikiliza

Annex 7.4: Statement from UNICEF Country Representative on behalf of UN agencies

SPEECH MADE BY Ms. MANIZA ZAMAN; UNICEF COUNTRY REPRESENTATIVE IN TANZANIA ON BEHALF OF UNITED NATIONS AGENCIES AT THE WORLD BREASTFEEDING WEEK (WBW), 1 - 7 August 2018

Honourable Minister of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children, Honourable Ummy Mwalimu
Permanent Secretary, Community Development, Gender, Elderly and Children, Dr. Mpoki Ulisubisya
Managing Director of Tanzania Food & Nutrition Centre, Dr Vincent Assey
Representatives from Government Ministries, Departments, Agencies, Regions and Councils
Representatives of Donor organization, UN Agencies, CSOs, and the Private sector
Representatives from the media
Distinguished guests
Ladies and Gentlemen,

Habari za Asubuhi!

I am delighted to be here with all of you today and speak on behalf of United Nations in Tanzania as we launch **World Breastfeeding Week 2018** with the theme **Breastfeeding: Foundation of Life**".

Firstly, the UN congratulates the **Government of Tanzania** for the steadfast commitment to improving the health and well-being of its citizens. This year's theme for World Breastfeeding Week reminds us of the importance of breast-feeding for child survival, prevention of malnutrition, child development, mother's health and wider societal benefits. The Government of Tanzania is sincerely commended for all its efforts to promote, protect and support mothers to optimally breastfeed.

A. Let us put today's event and topic in perspective. We are now in the third year of implementation of an ambitious set of global goals, the **Sustainable Development Goals (or SDGs)**, which Tanzania has signed up to. These goals are reflected in Tanzania's 5 Year Development Plan, Mkuza III in Zanzibar and several sectoral policies and plans. Breastfeeding is important for achieving **SDG 3 (ensuring healthy lives and promoting well-being for all)**. But not only that. Breast milk is the best source of nutrition for infants — and breastfeeding can be practiced universally. Therefore, encouraging and supporting women in **low-resource settings** to breastfeed can play a vital role in achieving **SDG 1 (end poverty)**, **SDG 2 (end hunger, achieve food security and improved nutrition)** and **SDG 10 (reduce inequality within and among countries)**.

The multiple benefits of breastfeeding are worth emphasizing. Science has re-affirmed that breastmilk contains **all the nutrients an infant needs in the first six months of life** and it protects babies and young children against a myriad of diseases and infections.

Tanzania is making great strides in reducing deaths among children under-five. However there are still an unacceptable number of preventable child deaths - a large number occurring in the first 28 days of life - or newborn period. Data shows that **Tanzania is one of the top ten countries with the highest numbers of new-born deaths in the world**. Each year, approximately 51,000 new-borns die, 22,000 of them in their first day of life.

In addition, we have the problem of malnutrition. We recognize that over the years there is progress is reducing malnutrition - but today **one in three Tanzanian children under five are stunted** - or suffering from chronic malnutrition.

For both these issues - child survival and combatting malnutrition - breast-feeding is key. Evidence shows that **breastfeeding protects children** against diarrhoea and common childhood illnesses such as pneumonia which often are the causes of death in children under five. Proper breastfeeding means proper nutrition for children - one key factor in combatting malnutrition. Breastfeeding also has longer-term health benefits, such as **reducing the risk of overweight and obesity** in childhood and adolescence, by at least 15%.

The benefits are not only for children. **When it comes to women's health**, we know that breastfeeding helps with birth spacing, reduces the risk of breast and ovarian cancer and hypertension.

Beyond the individual level, we should consider the benefits of breastfeeding for the countries. Here are 3 facts:

- Increased rates of breastfeeding means children will be healthier and less money has to spent on health care and treatment of illnesses.
- The Lancet series on breastfeeding published in 2016 show that optimal breastfeeding is also associated with **higher IQ** and results in economic benefits for the country.
- In 2017 the World Bank estimated that every \$1 invested in promoting optimal breastfeeding will generate \$35 in economic returns.

B. With all this evidence let us examine how Tanzania is faring.

The good news is that breastfeeding is a norm in Tanzania. Almost all Tanzanian children (98%) are breastfed for some time during their life. In fact **Tanzania has already achieved the World Health Assembly**

(WHA) target of at least 50% children 0-5 months receiving exclusive breastfeeding by 2025. This really is positive!

However, OPTIMAL breastfeeding remains a challenge.

Optimal breastfeeding, recommended by **WHO and UNICEF, means:**

- Early initiation of breastfeeding within 1 hour after birth;
- Exclusive breastfeeding for the first 6 months of life;
- Continued breastfeeding up to 2 years of age or beyond, with introduction of nutritionally adequate and safe complementary foods at 6 months.

According to TDHS 2015/16, only half (51%) of infants are breastfed within one hour after birth, and 14% are given water, infusions or other pre-lacteal feeds.

Over 40% of Tanzanian children do not yet benefit from exclusive breastfeeding for the first 6 months and are hence denied the best start in life.

When we examine some of the common barriers to breast-feeding the following emerge:

- a. The main bottleneck to optimal breastfeeding is not lack of knowledge among mothers, **but lack of support from their family entourage**, and especially their husbands.
- b. Most of Tanzanian **mothers are over-burdened with heavy demands on their time** - so prioritizing breastfeeding becomes difficult
- c. **Not enough attention is given to maternal nutrition during pregnancy and lactation** - and yet this is essential for a mother to breastfeed optimally
- d. In terms of provision of services, an analysis done in 2017, showed that only 34% of health service providers received training on promotion of optimal breastfeeding during **the last 5 years**; and only 18% of (male and female) caregivers of babies received counselling on optimal breastfeeding
- e. **Funding** - interventions to promote infant and young child feeding receive little funding from the LGAs and the Central Government budget. There is great reliance on donor funding for such programmes and so these can start and stop depending on donor support.

C. Ladies and gentlemen, in order to address some of these challenges, there are a few actions that will help Tanzania progress even more on optimal breastfeeding. These are:

- **Enforcement and monitoring** of the relevant good policies, legislation, guidelines that Tanzania already has
- Consider ratification of the ILO Maternity Protection Convention n. 183 of year 2000 which requires paid maternity leave of not less than 14 weeks (98 days). Currently *Employment and Labour Act of 2004* provides 84 days paid maternity leave, and breastfeeding breaks

- Improve **access to skilled breastfeeding counselling** in health facilities and also in communities
- Engage **more men** in the communities to share child care and domestic responsibilities so that mothers can practice optimal breastfeeding
- **Reach out to more young people** as future parents in understanding the benefits of optimal breastfeeding so that they adopt the good practices
- **Invest more in breastfeeding programmes** - putting more domestic resources will help expand coverage of programmes and make these interventions sustainable.

Before I end, **it is important to stress that no infant formula will be able to replicate the benefits of breastmilk and breastfeeding.** I have already spoken about the unparalleled nutritional value of breastmilk and longer term benefits to both the babies and mothers. Let us remember that the act of breastfeeding **also** creates a deep bond between the mother and the child, making the baby feel comfortable and safe - exactly what babies need for optimal development.

Hon Minister and distinguished guests, **United Nations Agencies are committed to continuing our support to health and nutrition programmes in Tanzania in line with the Government's priorities.** We will work with the Government and partners to promote, protect and support breastfeeding in every part of the country so that all children in Tanzania, irrespective of where they are born, get this best start to life.

ASANTENI SANA

Annex 7.5: Opening speech at media seminar

SEMINA YA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MAADHIMISHO WIKI YA UNYONYESHaji MWAKA 2018 MAZIWA YA MAMA DUNIANI

**Hotuba ya Ufunguzi ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Taasisi ya chakula na Lishe Tanzania
Dk. Vincent Assey,
19 Julai 2018**

Wadau wa Lishe,
Waandishi wa Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Ndugu wanahabari,
Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha wanahabari wote kwenye semina hii inayo husu Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama Duniani kama sehemu ya maadhimisho kitaifa.

Ndugu wanahabari,

Kama tunavyo fahamu, kuanzia tarehe 1 hadi 7 Agosti, kila mwaka Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama. Maadhimisho hayo ni fursa ya pekee katika kuunganisha nguvu za wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla ili kufikia malengo ya **Azimio la Innocenti** lililopitishwa mwaka 1992. Azimio hilo linaisitiza umuhimu wa kulinda, kuimarisha na kuendeleza unyonyeshaji wa maziwa ya mama. Kulinda, Kuimarisha na Kuendeleza unyonyeshaji ni muhimu ili kuwezesha wanawake waweze kutekeleza taratibu sahihi za unyonyeshaji ambazo ni:

- Kuanza kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama katika saa moja ya kwanza mara tu baada ya kujifungua.
- Kumnyonyesha mtoto anyonyeshwe mara kwa mara usiku na mchana kadiri ya uhitaji wake bila kupangiwa ratiba.
- Kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama pekee kuanzia anapozaliwa hadi anapotimiza umri wa miezi sita.
- Kutompa mtoto maji, vinywaji au chakula cha aina yeyote isipokuwa dawa na chanjo kwa ushauri wa mtoa huduma wa afya hadi atomize umri wa miezi sita.
- Kumwanzishia mtoto vyakula vya nyongeza, anapofikia umri wa miezi sita, lakini aendeleo kumnyonyesha maziwa ya mama hadi anapofikisha umri wa miaka miwili au Zaidi.

Ndugu wanahabari,

Madhumuni ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani kwa mwaka 2018 ni haya yafuatayo:

- **Kuitaarifu jamii** kuhusu uhusiano uliopo kati ya lishe bora, uhakika wa chakula, kupunguza umasikini na unyonyeshaji.
- **Kusisitiza** unyonyeshaji ni msingi wa maisha
- **Kushirikisha** watu binafsi, asasi za kiraia ili kuleta matokeo mazuri
- **Kuimarisha** hatua za kuhamasisha unyonyeshaji kwa lengo la kujenga jamii yenye lishe bora, uhakika wa chakula na kupunguza umasikini.

Kama ilivyo ada, kila mwaka, maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani hubeba kauli mbiu ambayo hulenga katika kulinda, kuimarisha na kuendeleza unyonyeshaji. Kauli mbiu ya mwaka huu 2018 ni: ***“Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama ni Msingi wa Maisha.”*** Kauli mbiu ya mwaka huu inasisitiza umuhimu wa maziwa ya mama kwa afya na uhai wa mama na mtoto. Inashauriwa kuwa mama anyonyeshe mtoto wake maziwa yake pekee katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo, na apewe chakula cha nyongeza anapotimiza miezi sita, huku akiendelea kunyonyeshwa hadi kufikia miaka miwili au zaidi. Hivyo basi, ni muhimu kwa mama kupata msaada katika jamii husika kwa wakati na pamoja na

kupata elimu ya afya na unyonyeshaji unaofaa kutoka katika vituo vinavyotoa huduma ya afya.

Uyonyesha ni jukumu la kila mtu katika nafasi yake, wadau hao ni pamoja na familia, viongozi ngazi ya jamii, wafanyakazi wa afya wenye ujuzi, wataalamu wa masuala ya unyonyeshaji na marafiki. Ni vizuri kwa mama kupata muda na msaada wa kutosha katika kipindi cha kunyonyesha na pia apate elimu ya makuzi na malezi kwa mtoto wake. Hivyo basi ili kuufanya unyonyeshaji uwe endelevu mama anahitaji msaada toka kwa kila mwana jamii na hasa mama apate unasihi wa maswala ya unyonyeshaji toka kwa mhudumu wa afya ya jamii kuweza kumsaidia kutatua changamoto za ulishaji wa mtoto wake.

Ndugu wanahabari,

Wiki ya Unyonyeshaji Duniani kwa mwaka 2018 imeweka msisitizo zaidi katika mambo yafuatayo :

Kuzuia aina zote za utapiamlo

Utapiamlo unajumuisha matatizo ya upungufu wa virutubishi mwilini (kwa mfano ukondefu) na matatizo ya kuzidi kwa virutubishi mwilini (kwa mfano uzito uliozidi) unaambatana na magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza yenye uhusiano na masuala ya ulaji na mitindo ya maisha. Kuwepo kwa aina hizi mbili za utapiamlo kwa pamoja katika nchi yetu kunaleta athari muda mfupi na za muda mrefu za kiafya, kiuchumi na kijamii , siyo tu kwa waathirika, bali pia kwa familia zao, jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa muda mrefu imejulikana kwamba utapiamlo hususani uzito pungufu pamoja na udumavu ni matatizo yaliyojikita kwenye nchi nyingi zenye kipato cha chini ikiwemo Tanzania. Kwa sasa tatizo la uzito uliozidi ambalo huambatana na magonjwa sugu na yasiyo ya kuambukiza linaongezeka kwa kasi katika jamii yetu hivyo kufanya tatizo la utapiamlo kuongeza .

Kuhakikisha kuwepo kwa uhakika wa chakula hata wakati yanapotokea majanga

Uhakika wa chakula ni kuwepo kwa hali nzuri ya upatikanaji endelevu wa chakula kwa watu wote na wakati wote. Uhakika wa chakula unachangiwa na upatikanaji wa chakula pia uwezo wa kumudu gharama za kununua chakula hicho.

Taratibu sahihi za ulishaji watoto wachanga na wadogo zinaleta faida za kiafya na ustawi kwa wanawake na watoto katika maisha yao yote.

Shirika la Afya Duniani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto na kupitia Wizara yetu ya *Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto* wanapendekeza:

- Kuanza kunyonyesha mtoto maziwa ya mama mapema katika kipindi kisichozidi saa moja baada ya kujifungua.

- Kunyonyesha maziwa ya mama pekee bila kumpa mtoto maji, kinywaji au chakula kingine katika miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa. Mtoto apewe chanjo, dawa na matibabu mengine kwa ushauri wa watoa huduma za afya.
- Kumwanzishia mtoto vyakula vya nyongeza anapotimiza umri wa miezi sita. Kuendelea kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama hadi atimize umri wa miezi 24 (miaka miwili) au zaidi.

Kuvunja mzunguko wa umasikini

Umasikini unachangiwa na masuala mbalimbali ikiwemo njaa na utapiamlo. Njaa husababisha uchumi wa familia maskini kuporomoka, hivyo kuzisababishia familia hizo kushindwa kuvunja mzunguko wa umasikini. Dunia endelevu inaanza kwa kutokomeza umasikini wa kila aina na mahali popote Kulingana na mtafiti aitwaye *Pinstrup-Andersen* “siyo kila mtu masikini anatatizo la njaa, lakini karibu kila mtu mwenye njaa ni masikini “Mamilioni ya watu wanaishi katika hali ya njaa na utapiamlo kwa sababu tu hawana uwezo wa kununua chakula cha kutosha, kupata chakula ambacho kinavirutubishi vya kutosha au hawana uwezo wa kupata pembejeo wanazohitaji kwa ajili ya kulima chakula cha kutosheleza mahitaji yao wenyewe.”

Kunyonyesha maziwa ya mama kunaimarisha afya na ustawi wa wanawake na watoto na ni msingi wa maendeleo ya nchi na mstakabali wake wa baadaye pia ni njia ambayo inaleta usawa mkubwa katika kuvunja mzunguko wa umaskini nchini.

Unyonyeshaji watoto maziwa ya mama huzuia aina zote za utapiamlo, uhakikisha uhakika wa chakula kwa watoto wachanga na wadogo, na hivyo husaidia kuondoa watu na taifa katika njaa na mzunguko wa umasikini. Kwa hiyo unyonyeshaji ni msingi wa maisha. Kulinda, kuendeleza na kuimalisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama ni jambo lenye umuhimu katika kujenga dunia na Tanzania endelevu

Ndugu wanahabari,

Kwa kutambua ukweli huo Serikali ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali Kulinda, Kuimarisha na Kuendeleza unyonyeshaji. Hatua hizo ni pamoja na

- KutungaSheria ya Ajira na Mahusiano kazini ya mwaka 2004 inayotambua kuwa unyonyeshaji ni haki ya mtoto na hivyo hutoa mafao mbalimbali ya uzazi ili kuwawezesha wanawake kumlea mtoto hususani kumnyonyesha ipasavyo. Mama mwajiriwa aliyejifungua mtoto anahaki ya kupata likizo ya siku 84 (iwapoamejifungua mtoto mmoja) AU siku 100 (iwapo amejifungua zaidi ya mtoto mmoja). Aidha, baba pia hupata likizo ya ubaba ya siku tatu katika wiki moja ya kwanza baada ya mkewe

kujifungua. Pia seria hiyo inampa mama anayenyonyesha ruhusa ya saa mbili kila siku ili akamnyonyeshe mtoto wake.

- Aidha kwa mujibu wa sheria mwajiri haruhusiwi kumpangia mama mjamzito au anayenyonyesha kazi ngumu au za hatari kwa afya yake yeye mwenyewe au afya ya mtoto, kumpangia kazi za usiku au unyanyasaji wa aina yoyote.
- Changamoto iliyopo katika suala hili ni wanawake wengi kufanya kazi katika sekta isiyokuwa rasmi, kazi binafsi, na kilimo. Huko, hawafaidiki na likizo ya uzazi. Hivyo ni wajibu wa wanajamii, hususani wanaume kuliangalia suala hili kwa makini ili wanawake wenye watoto wachanga wapewe fursa ya kupumzika na kuwanyonyesha watoto wao kikamilifu hususani katika miezi sita ya mwanzo baada ya kujifungua.
- Nchi yetu pia imetunga sheria mbalimbali zinazolinda haki ya afya na lishe kwa mama na mtoto. Miongoni kwa sheria hizo ni: Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inayotambua kuwa chakula ikiwa pamoja na unyonyeshaji ni haki ya mtoto. Pia kuna Kanuni inayodhibiti Uzaji wa Maziwa Mbadala na Bidhaa zinazoambatana na maziwa hayo ya mwaka 1994, na kufanyiwa maboresho mwaka 2013.
- Aidha, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizo ridhia mikataba mbambali ya kimataifa na kuiwekea mazingira ya kisheria ili kuwezesha utekelezaji wake katika kulinda haki na afya ya mama na mtoto. Miongoni mwa mikataba hiyo ni pamoja na:
 - Mkataba wa Kulinda Haki za Uzazi wa Shirika la Kazi Duniani
 - Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto
 - Kanuni ya Kimataifa ya Kudhibiti Uzaji na Usambazaji wa Vyakula Mbadala vya Watoto Wachanga.

Ndugu wanahabari,

Sote tunatambua mchango wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa, kuelimisha na pia kuburudisha. Lakini kwa miaka ya hivi karibuni dhima hiyo imepanuka na kujumuisha masuala ya ufuatiliaji, kupaza sauti za watu wasio na sauti katika jamii, kusaidia kulinda maslahi ya jamii na mambo mengine mengi. Vyombo vya habari vina weza kuendelea kuhabarisha, kuelimisha kuhusu umuhimu na taratibu sahihi za unyonyeshaji kama vile kuanzisha kunyonyesha mtoto ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama pekee katika miezi sita bila kumpa kitu kingine chochote, kumnyonyesha mtoto kila anapohitaji na kuendelea kumnyonyesha hadi anapofikisha miaka miwili au zaidi.

Hali-kadhalika, vyombo vya habari vinaweza kufuatilia utekelezaji wa sheria mbalimbali zinazolinda haki za uzazi na ulishaji wa watoto kwa kufanya tafiti, kuandika au kuripoti matukio mbalimbali kama vile utekelezaji wa haki mbalimbali ikiwemo haki ya kupata likizo ya uzazi. Aidha, vyombo vya habari vinaweza kutoa taarifa sahihi kuhusu

unyonyeshaji na ulishaji wa watoto kwa ujumla, hivyo kupambana na imani potofu kuhusu unyonyeshaji, taarifa zisizo sahihi zinazolenga maslahi ya kibishara ya maziwa mbadala na vyakula vya watoto- na hivyo kuchangia uboreshaji wa lishe na afya ya mama na motto, kujenga taifa lenye nguvukazi imara yenye tija, kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu na ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Ndugu Wanahabari,

Ninyi ni miongoni mwa wadau wakuu wa mawasiliano yanayolenga kubadili mitazamo na tabia za jamii kuhusu masuala ya lishe na afya. Nina uhakika kwamba baada ya semina hii mtakuwa na uelewa mpana zaidi kuhusu masuala ya lishe na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo. Nendeni mkatumie yale mtakayojifunza ili kuendelea kutoa taarifa sahihi na kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya lishe. Taifa letu lina wahitaji sana katika juhudi za kupambana na adui maradhi. Kalamu, kamera, sauti, ubunifu na weledi wenu ni nyenzo bora zenye ufanisi mkubwa katika kupambana na utapiamlo na kujenga Tanzania yenye watu wenye afya bora.

Kwa maneno hayo nawakaribisheni sana kwenye Taasisi yetu. Naomba sasa kutangaza kuwa semina ya Waandishi wa Habari kuhusu Wiki ya Unyonyeshaji Duniani mwaka 2018 imefunguliwa rasmi.

Annex 7.6: Concept note

**DHANA YA WIKI YA UNYONYESHAJI WA MAZIWA
YA MAMA DUNIANI MWAKA 2018**



KAULI MBIU: “Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama ni Msingi wa Maisha”

1.0 Utangulizi

Kila mwaka kuanzia tarehe 1 hadi 7 Agosti, Tanzania huungana na nchi nyingine kuadhimisha Wiki ya Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama Duniani. Maadhimisho hayo yana lengo la kusisitiza umuhimu wa kulinda, kuimarisha na kuendeleza unyonyeshaji wa maziwa ya mama na pia kuweka msukumo wa kipekee katika kuunganisha nguvu ya wadau mbalimbali ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Maadhimisho hayo huambatana na kauli mbiu maalum zinazolenga kuhamasisha na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa watoto na taratibu sahihi za ulishaji watoto wachanga na wadogo. Hii husaidia kukabiliana na tatizo la utapiamlo nchini na hasa udumavu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kauli mbiu ya mwaka huu 2018 ni: ***“Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama ni Msingi wa Maisha”***. Pia maadhimisho haya hutoa fursa nzuri kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kutoa uamuzi na kulipa kipaumbele suala zima la unyonyeshaji na hivyo kulifanya ni ajenda katika mikutano mbalimbali na kutenga raslimali fedha ili kuweza kutekeleza afua zinazohusu ukuaji na maendeleo ya mtoto. Maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama ni fursa muhimu ya kutoa hamasa kwa jamii katika kulinda, kuimarisha na kuendeleza unyonyeshaji. Unyonyeshaji ni suluhisho ambalo linampa kila mtu msingi imara wa mwanzo wa maisha. Husaidia katika kuboresha afya na ustawi wa wanawake na watoto duniani kote.

1.2 MALENGO YA WIKI YA UNYONYESHAJI DUNIANI 2018

Mwaka huu 2018 malengo ya unyonyeshaji ni:

- **Kuitaarifu jamii** kuhusu uhusiano uliopo kati ya lishe bora, uhakika wa chakula, kupunguza umasikini na unyonyeshaji.
- **Kusisitiza** unyonyeshaji ni msingi wa maisha
- **Kushirikisha** watu binafsi, asasi za kiraia ili kuleta matokeo mazuri
- **Kuimarisha** hatua za kuhamasisha unyonyeshaji kwa lengo la kujenga jamii yenye lishe bora, uhakika wa chakula na kupunguza umasikini.

1.3 Kauli mbiu ya Wiki ya Unyonyeshaji kwa mwaka 2018

Kauli mbiu ya mwaka huu inasisitiza umuhimu wa maziwa ya mama kwa afya na uhai wa mama na mtoto. Inashauriwa kuwa mama anyonyeshe mtoto wake maziwa yake pekee katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo, na apewe chakula cha nyongeza anapotimiza miezi sita, huku akiendelea kunyonyeshwa hadi kufikia miaka miwili au zaidi. Hivyo basi, ni muhimu kwa mama kupata msaada katika jamii husika kwa wakati na pamoja na kupata elimu ya afya na unyonyeshaji unaofaa kutoka katika vituo vinavyotoa huduma ya afya.

Uyonyesha ni jukumu la kila mtu katika nafasi yake, wadau hao ni pamoja na familia, viongozi ngazi ya jamii, wafanyakazi wa afya wenye ujuzi, wataalamu wa masuala ya unyonyeshaji na marafiki. Ni vizuri kwa mama kupata muda na msaada wa kutosha katika kipindi cha kunyonyesha na pia apate elimu ya makuzi na malezi kwa mtoto wake. Hivyo basi ili kuufanya unyonyeshaji uwe endelevu mama anahitaji msaada toka kwa kila mwana jamii na hasa mama apate unasihi wa maswala ya unyonyeshaji toka kwa mhudumu wa afya ya jamii kuweza kumsaidia kutatua changamoto za ulishaji wa mtoto wake.

1.4 Kwa nini tunaadhimisha wiki ya Unyonyeshaji?

Takwimu kutoka maeneo yote duniani zinaonesha kuwa kiwango cha watoto wanaoanzishiwa kunyonya maziwa ya mama kwa wakati sahihi ni vya kuridhisha, ni asilimia 40 tu ya watoto wote wenye umri chini ya miezi sita hunyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji, vinywaji au vyakula vingine, na ni asilimia 45 tu huendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama hadi wanapofikisha umri wa miaka miwili. Zaidi ya hayo, kuna tofauti kubwa za takwimu za unyonyeshaji kikanda pia kati ya nchi moja na nyingine na hata kati ya mkoa mmoja na mwingine ndani ya nchi. Tunapotoa msukumo katika unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa kufuata taratibu sahihi huzuia vifo vya watoto zaidi ya wapatao 823 000 na vifo 20 000 vya wanawake vinavyotokana na uzazi kila mwaka. Pia, kutonyonyesha watoto maziwa ya mama kunapunguza uwezo wa kiakili wa watoto na kusababisha hasara kiuchumi ambapo dunia hupoteza takribani dola za kimarekani 302 bilioni kila mwaka.

Tanzania imefanya juhudi kubwa katika Ulishaji wa watoto wachanga na wadogo, lakini mpaka sasa hali hairidhishi kama takwimu za mwaka 2015/16 zinavyoonyesha. Utafiti wa Hali ya Afya na Demografia wa mwaka 2015/16 unaonyesha kuwa katika kila wanawake 10 wanaonyonyesha 9 wananyonyesha watoto wao, lakini unyonyeshaji huo haufanyiki kama inavyostahili. Wanawake 5 tu kati ya 10 wanaojifungua hunyonyesha watoto wao katika saa moja ya mwanzo na wanawake 6 kati ya 10 huendelea kunyonyesha maziwa ya mama pekee katika miezi sita ya mwanzo.

Hata hivyo utafiti huo unaonyesha kuwa watoto 4 kati ya 10 wenye umri chini ya miezi sita hupewa vinywaji au vyakula vingine mbali na maziwa ya mama. Watoto 3 kati ya hao (10) hupewa vinywaji kwa kutumia chupa za kulishia watoto. Takwimu pia zinaonyesha kuwa ni asilimia 8 tu ya watoto walio katika umri wa miezi 6-23 hupewa vyakula vya nyongeza kwa kuzingatia vigezo muhimu vya umri, kiasi, idadi ya milo kwa siku, uzito na ulaini wa chakula na mchanganyiko wa vyakula mbalimbali ikiwa ni pamoja na chakula cha asili ya wanyama. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 90 ya watoto wenye umri kati ya miezi 6-8 wanakuwa wamepata

vyakula vya nyongeza na asilimia 97 ni kwa watoto wenye umri kati ya miezi 9-11.

Ni ukweli usiopingika kuwa Maziwa ya mama ni chakula maalumu ambacho kimetengenezwa kukidhi mahitaji ya lishe na kingamwili kwa mtoto. Unyonyeshaji ni njia asilia ya ulishaji watoto na huimarisha uhusiano baina ya mama na mtoto, katika mazingira na hali yeyote ya kiuchumi na kijamii. Kuna vikwazo vingi vinavyoathiri mazingira yanayoweza wanawake kunyonyesha watoto wao. Baadhi ya vikwazo hivyo ni pamoja na kuwa na huduma hafifu za afya na lishe hususani katika ngazi ya jamii, wanawake wanaonyonyesha kukosa msaada katika ngazi ya familia, jamii na mahala pa kazi, na hata baadhi ya waajiri kutokutekeleza sera za kazi zinazolenga kuwawezesha wanawake kuwanyonyesha na kuwalisha watoto wao. Sababu nyingine ni wafanyabiashara wa maziwa mbadala, vyakula vya watoto wachanga na wadogo na bidhaa zinazoambatana navyo kutozingatia Kanuni zinazosimamia Usambazaji na Uzaji wa vyakula hivyo katika nchi yetu.

Kutokana na changamoto hizi, juhudi za pamoja zinahitajika ili kuweza kufikia lengo la Baraza la Afya Duniani. Lengo hilo ni kufikia angalao asilimia 50 ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji, vinywaji au vyakula vingine ifikapo mwaka 2025.

Ingawa tumeweza kupiga hatua katika kuboresha viwango vya unyonyeshaji, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuondoa mapungufu yaliyopo kati sera na mikakati ya utekelezaji. Sote tunapaswa kuhamasisha unyonyeshaji ikiwa ni mojawapo ya mkakati wa kuboresha lishe ya jamii, kuimarisha uhakika wa chakula na kupunguza umasikini.

2.0 Wiki ya Unyonyeshaji Duniani kwa mwaka 2018 imeweka msisitizo zaidi katika :

2.1 Kuzuia aina zote za utapiamlo

Utapiamlo unajumuisha matatizo ya upungufu wa virutubishi mwilini (kwa mfano ukondefu) na matatizo ya kuzidi kwa virutubishi mwilini (kwa mfano uzito uliozidi) unaambatana na magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza yenye uhusiano na masuala ya ulaji na mitindo ya maisha. Kuwepo kwa aina hizi mbili za utapiamlo kwa pamoja katika nchi yetu kunaleta athari muda mfupi na za muda mrefu za kiafya, kiuchumi na kijamii, siyo tu kwa waathirika, bali pia kwa familia zao, jamii na taifa kwa ujumla. Kwa muda mrefu imejulikana kwamba utapiamlo hususani uzito pungufu pamoja na udumavu ni matatizo yaliyojikita kwenye nchi nyingi zenye kipato cha chini ikiwemo Tanzania. Kwa sasa tatizo la uzito uliozidi ambalo huambatana na magonjwa sugu na yasiyo ya kuambukiza linaongezeka kwa kasi katika jamii yetu hivyo kufanya tatizo la utapiamlo kuongeza.

Utapiamlo miongoni mwa watoto hususani ukondefu, kwa kawaida husababishwa na ulishaji watoto vyakula mbadala ambavyo havina virutubishi vya kutosha na watoto hupewa kiasi kidogo na idadi ya milo

huwa michache ukilinganisha na umri wa mtoto. Hali huweza kuwa mbaya zaidi hususani katika familia zenye kipato cha chini. Ukondefu unaweza kuzuiwa kwa njia mbalimbali, kwa mfano kwa kuzuia tatizo la kuhara, kuzingatia taratibu sahihi za ulishaji wa watoto ikiwa ni pamoja na kuwaanzishia watoto vyakula vya nyongeza kwa wakati wanapotimiza umri wa miezi sita, kuzingatia kiasi na chakula, idadi ya milo kwa siku. Uwezekano wa kupata uzito uliozidi na kiribatumbo kwa mtoto huongezeka maradufu kadri mtoto anapolishwa vyakula mbadala kwa chini ya miezi sita, na tatizo hili limeanza kujitokeza katika jamii na mazingira mbalimbali hapa nchini.

Kwa kiasi kikubwa unyonyeshaji pia unahusishwa na lishe ya mama mjamzito na anayenyonyesha. Hali nzuri ya lishe ya mama mjamzito humsaidia kuufanya mwili uwe na hifadhi ya kutosha la tabaka la mafuta na hivyo kujiandaa vema kwa unyonyeshaji mara anapojifungua. Dhana inayojengwa kuwa mama anapata utapiamlo na kupungua uzito kutokana na kunyonyesha ni dhana potofu. Hivyo mama anahitaji kupata mlo mmoja wa ziada wakati wa unjauzito na hata baada ya kujifungua ili aweze kukidhi mahitaji yake na ya mtoto wake. Lishe bora ya mama ya mjamzito pamoja na kupanga uzazi na matumizi ya huduma za kisasa za uzazi wa mpango ni mambo ya msingi yanayosaidia kuzuia utapiamlo na kuufanya mwili wa mama ujengeke vema kabla ya kupata ujauzito mwingine. Unyonyeshaji watoto maziwa ya mama pekee pia humsaidia mama kurudia hali yake ya uzito wa kawaida sawa sawa na uzito aliokuwa nao kabla ya ujauzito.

Takwimu zinaonyesha ulimwenguni, kuna watoto takribani milioni 155 wa umri chini ya miaka 5 ambao wamedumaa, milioni 52 wanaukondefu na milioni 41 wanauzito uliozidi. Inakadiliwa kuwa unyonyeshaji wa maziwa ya mama unaweza kupunguza athari za uzito uliozidi na uzito uliokithiri kwa takribani asilimia 10% ikilinganishwa na maziwa mbadala. Vilevile takwimu za kimataifa zinaonyesha kuwa, zaidi ya watu wazima bilioni 1.9 (Wenye umri zaidi ya miaka 18 na zaidi) walikuwa na uzito uliozidi. Kati ya hawa zaidi ya watu milioni 650 walikuwa na uzito uliokithiri. Katika nchi zinazoendelea na zile zenye uchumi wa kati, watoto walionyonyeshwa maziwa ya mama walikuwa katika hatari ndogo ya kufa kwa asilimia 21% ndani ya mwaka wa kwanza wa kuzaliwa, ikilinganishwa na watoto ambao hawakunyonyeshwa kabisa.

Nchini Tanzania, takwimu za TDHS 2015/16 zinaonyesha idadi ya watoto waliodumaa ni milioni 2,700,000; uzito pungufu 340,000 na ukondefu 160,000.

Kutokana na takwimu hizi kuna ushahidi mkubwa wa faida za unyonyeshaji kwa pande zote kwa mama na mtoto na faida hizo ni:

Mama: Humsaidia kupangilia uzazi, kupunguza uwezekano wa kupata saratani ya matiti na via vya uzazi, kuzuia upotevu wa kiwango kikubwa

cha damu baada ya kujifungua, na kupunguza uwezekano wa kupata tatizo la shinikizo kubwa la damu.

Mtoto: Maziwa ya mama yanakinga mwili ambazo humsaidia kupambana na maambukizo ya magonjwa, kupunguza kasi ya kuugua mara kwa mara hususani ugonjwa wa kuharisha, maambukizi kwenye mapafu na mfumo wa njia ya hewa, na maambukizi kwenye masikio, kuzuia magonjwa ya meno na kuboresha ukuaji wa mwili na akili hivyo kuinua kiwango cha akili ya mtoto katika kujifunza na utambuzi wa masuala mbalimbali.

2.2 Kuhakikisha kuwepo kwa uhakika wa chakula hata wakati yanapotokea majanga

Uhakika wa chakula ni kuwepo kwa hali nzuri ya upatikanaji endelevu wa chakula kwa watu wote na wakati wote. Uhakika wa chakula unachangiwa na upatikanaji wa chakula pia uwezo wa kumudu gharama za kununua chakula hicho. Pia kuna mambo mengine yanayoathiri uhakika wa chakula ikiwa ni pamoja na njaa, majanga mbalimbali ya kiasili kama vile ukame, hali ya kiusalama katika jamii ikiwemo vita na machafuko yanayoathiri amani, na uharibifu wa mazingira.

